TANGAZO LA SERIKALI NA. 380 la tarehe 15/5/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

SURA. 287

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA UVUNAJI WA MAJI YA MVUA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME ZA MWAKA 2020

Jina la sheria

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Uvunaji wa Maji ya Mvua ya Halmashauri ya Wilaya Same ya Mwaka 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama itakapoelezwa vinginevyo:-

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same au afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"uvunaji wa maji ya mvua" maana yake ni kukusanya na kutunza maji ya mvua kutoka kwenye ardhi, miamba au kutoka kwenye paa la nyumba kwa kutumia teknolojia rahisi ya makinga maji.

Wajibu wa mmiliki wa jengo

3. Kila mmiliki wa jengo la kudumu linalojengwa katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Same atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba anajenga miundombinu ya kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi katika vyombo maalum au tanki.

Wajibu wa taasisi za Serikali

4. Kila taasisi ya Serikali inayomiliki majengo yake yenyewe itakuwa na wajibu wa kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua.

Utaratibu wa utoaji vibali vya ujenzi

5. Halmashauri, kabla ya kutoa kibali cha ujenzi itakuwa na wajibu wa kuhakikisha michoro ya ujenzi inayoombewa kupatiwa kibali inayo miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua.

Uwezo wa Afisa Mwidhini wa

6.- (1) Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wa saa za kazi kukagua ujenzi wa miundombinu ya kuvunia maji ya mvua pamoja na vyombo vya kuhifadhia maji hayo.

(2) Afisa mwidhiniwa anaweza kuzuia kuendelea kwa ujenzi katika hatua yoyote ya ujenzi endapo atagundua kuwa nyumba inayojengwa haikuwekewa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua.

Miundombinu ya kuvunia maji

7. (1) Kila mtu au taasisi inayojenga miundombinu ya kuvunia maji ya mvua atatakiwa kuhakikisha kwamba inafuata viwango vitakavyoelekezwa na afisa mwidhiniwa.

(2) Ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua itakuwa ni ile ya teknolojia rahisi ambayo itamwezesha kila mtu kumudu gharama ya ujenzi.

(3) Matanki ya kuhifadhia maji ya mvua yatajengwa kwa saruji na ukubwa wake utazingatia mahitaji ya kaya au taasisi na yatatakiwa kufunikwa juu.

Majengo ya zamani

8. Kila mmiliki wa jengo lililopo katika eneo la Halmashauri ambalo lilijengwa kabla ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hii atatakiwa kuhakikisha kuwa, anajenga miundombinu ya kuvuna na kuhifadhia maji ya mvua.

Visima vya maji

9. Visima vyote vilivyochimbwa kwa madhumuni ya kuvuna maji ya mvua vitatakiwa kujengwa kitaalam kwa zege nzito au kwa namna nyingine ambayo itahifadhi maji bila kuhatarisha usalama wa wakazi au watumiaji wa visima husika.

Ukaguzi

10. Halmashauri inaweza kufanya ukaguzi katika taasisi za serikali, taasisi binafsi, taasisi za dini, asasi za kiraia au makazi ya wananchi ili kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Elimu ya uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua

11. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kutoa elimu kwa wananchi, taasisi za serikali, taasisi binafsi, asasi za kiraia na taasisi za dini juu ya-

(a) uchimbaji bora wa visima vya kuvunia maji ya mvua na maeneo yanayoruhusiwa hasa kwa majengo ambayo tayari yameshajengwa;
(b) uhifadhi bora wa maji ya mvua;
(c) uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia matenki makubwa ya plastiki; na
(d) kutibu maji ya mvua.

Makosa na Adhabu

12. Mtu atakuwa ametenda kosa endapo-

(b) Anajenga au ameanza ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua bila kupata kibali cha Halmashauri;
(c) amejenga jengo ambalo mchoro wake hauonyeshi miundombinu ya kuvuna maji ya mvua.

(2) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya kifungu kidogo (1) na akatiwa hatiani atalipa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufiliili sha

13. - Mkurugenzi anaweza kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote anayekiri kwa maandashi kutenda kosa

kosa

chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 13*)

KUFLILISHA KOSA

Mimi………………………………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same kwamba tarehe ………Mwezi………...Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo ya Uvunaji wa Maji ya Mvua ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi ------------------na kutekeleza wajibu niliopewa na Sheria Ndogo hii badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWA HIARI KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe………………………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo…………………………………….

Saini………………………………………Tarehe……………………………………

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Same umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa na mkutano wa baraza la Madiwani ulioitishwa tarehe 15/3/2018.

ANNA CLAIRE SHIJA
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Same*

CHRISTOPHER M. IRIRA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,Same*

NAKUBALI,

L.S

*Dodoma,*
16 Aprili, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*WN OR-TAMISEMI*
*Dodoma*